

HALMASHAURI YA WILAYA YA MLELE



TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mlele Alexius Kagunze amewaagiza walimu katika Halmashauri kuacha tabia ya kufanya kazi kwa mazoea hali inayopelekea baadhi ya shule kufanya vibaya katika mitihani ya kiwilaya, kimkoa na kitaifa.

Hayo ameyasema wakati akitembelea Shule ya Msingi Kusa wilayani humo kwa lengo la kubaini na kutafuta ufumbuzi wa changamoto zinazosababisha baadhi ya shule za msingi kufanya vibaya katika mitihani mbalimbali.

Akiongea na walimu shuleni hapo aliyataja baadhi ya mambo yanayosababisha baadhi ya shule kufanya vibaya katika mitihani kuwa ni pamoja na tabia ya walimu kufanya kazi kwa mazoea kama kulewa na kufanya shughuli binafsi wakati wa vipindi ama muda wa kazi.

Nao walimu kwa upande wao walizitaja baadhi ya changamoto wanazokabiliana nazo katika utendaji wa kazi kuwa ni pamoja na uhahaba wa vyumba vya madarasa, ambapo shule hiyo ina vyumba vya madarasa sita ikiwa na wanafunzi wa darasa la awali mpaka la saba hali inayopelekea baadhi ya madarasa kusoma kwa kubadilishana.

Changamoto nyingine ni uhaba wa vitendea kazi, kama vile vitabu, kompyuta kwa somo la tehama, umeme, nyumba za walimu, maji, madarasa kutokuwa na sakafu na uhaba wa walimu hali inayopelekea mwalimu mmoja kufundisha zaidi ya vipindi arobaini na nane kwa wiki.

Aidha Mkurugenzi amewaahidi walimu shuleni hapo kuwa atakabiliana na changamoto zilizo chini ya uwezo wake kama vile kutoa kipaombele kwa shule hiyo wakati wa mgawanyo wa walimu, kuongeza vyumba vya madarasa, kupeleka kompyuta moja kwa ajili ya somo la tehama.

Shule ya msingi kusa ni miongoni mwa shule 13 za msingi wilayani humo ambapo kiwilaya imekuwa katika kundi la tatu mbovu ikifuatiwa na shule ya msingi wachawaseme na ilela.

SEBASTIAN HAULE

AFISA HABARI HALMASHAURI (W)

MLELE